

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA ELIMU TANZANIA



Simu : +255735041168
: +255735041170
Barua pepe: director.general@tie.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:

Eneo la Mikocheni,
132 Barabara ya Ali Hasan Mwinyi,
S. L. P. 35094,
14112 DAR ES SALAAM.

09.08.2024

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA MALI CHAKAVU

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatarajia kufanya mnada wa hadhara wa mali chakavu (Magari 3, Pikipiki za miguu mitatu 2, Pikipiki ya miguu miwili 1, Mashine za kupiga Chapa 23, Samani za ofisi, Vifaa vya ofisi, na Vifaa vya TEHAMA. Vifaa hivyo viko katika ofisi za TET Makao Makuu – DSM, na Vituo vya Mikocheni, Press A, Press B, pamoja na Vituo vya Msamvu - Morogoro, Elimu ni Bahari - Tabora na Kisomo - Mwanza.

Aina ya Magari, Pikipiki na Vifaa vingine vitakavyouzwa na mahali vilipo ni kama ifuatavyo:

Na.	Kituo/Mkoa	Aina ya Gari/Pikipiki/Kifaa	Tarehe ya Mnada
1.	TET Makao Makuu (DSM)	<ul style="list-style-type: none">• SU 36648 NISSAN PATROL• SU 38719 FORD EVEREST• SU 37596 Bajaj (Miguu Mitatu)• SU 37595 Bajaj (Miguu Mitatu)• Samani za Ofisi• Vifaa vya TEHAMA• Vifaa Vingine	24.08.2024
2.	TET (Press A na Press B)	<ul style="list-style-type: none">• Mashine za kupiga Chapa na Mitambo mbalimbali• Vifaa Vingine	24.08.2024
3.	TET Morogoro (Viwanja vya S/M Msamvu)	<ul style="list-style-type: none">• Mashine za kupiga Chapa na Mitambo mbalimbali• Samani za Ofisi• Vifaa vya TEHAMA• Vifaa Vingine	26.08.2024

4.	Elimu ni Bahari - Tabora	<ul style="list-style-type: none"> • STG 3730 SUZUKI 125 - MOTOR-CYCLE • Samani za Ofisi • Vifaa vya TEHAMA • Vifaa Vingine 	28.08.2024
5.	Kisomo – Mwanza (Ndani ya Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Mwanza)	<ul style="list-style-type: none"> • STJ 7956 SUZUKI SAMURAI JX • Samani za Ofisi • Vifaa vya TEHAMA • Vifaa Vingine 	30.08.2024

Masharti ya Mnada ni kama ifuatavyo:

- i. Magari, Pikipiki na Vifaa vingine chakavu vitauzwa kama vilivyo na mahali vilipo.
- ii. Mnunuzi atakuwa ni yule atakayetamka bei ya juu kuliko wote kabla ya nyundo kupigwa.
- iii. Vifaa chakavu vitauzwa kwa fedha taslimu na malipo kufanyika kwa asilimia 100 papo hapo kupitia Namba ya Malipo (Control Number) itakayotolewa na Taasisi. Aidha mteja atatakiwa kuondoa vifaa alivyonunua siku hiyo hiyo ya mnada.
- iv. Mnunuzi wa Gari, Pikipiki na Mitambo atatakiwa kulipia papo hapo amana ya asilimia 25 ya bei aliyotaja, na asilimia inayobaki itatakiwa kulipwa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi na amana iliyolipwa haitarudishwa. Aidha mali itauzwa upya.
- v. Mnunuzi wa Gari, Pikipiki na Mitambo atatakiwa kuondoa/kuchukua mali aliyonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
- vi. Ruhusa ya kuangalia vifaa hivyo itatolewa siku mbili (2) kabla ya mnada kwa kila Kituo kuanzia **saa 4.00 asubuhi** hadi **saa 9.30 jioni**.
- vii. Mnada utafanyika kuanzia **saa 4.00 asubuhi** kwa kila Kituo kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu.

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU
TAASISI YA ELIMU TANZANIA